Nambari ya Mtahiniwa ____________________

SMZ

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA

133 KISWAHILI

MUDA : SAA 2.00 __ _________ ALHAMISI 29 NOVEMBA, 2018 mchana

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, maswali MANNE (4) kutoka sehemu B, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Simu za mkononi haziruhusiwi ndani ya chumba cha mtihani.

| KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI | | |
|---|---|---|
| NAMBARI YA SWALI | ALAMA | SAINI |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| 11. | | |
| 12. | | |
| JUMLA | | |

Mtihani huu una kurasa 12 zenye maandishi

Nambari ya Mtahiniwa ______________________

SEHEMU A: (Alama 15)

## UFAHAMU

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

Soma habari hii kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata.

Mabadiliko ya hali ya hewa yamekuwa makubwa kwa kiasi cha kutisha. Zamani mababu zetu walitabiri mvua wao wenyewe pasi na kuwa na vyombo vya kisasa. Suala linalozungumziwa sana siku hizi ni mabadiliko ya hali ya hewa na athari zake kwa jamii nzima. Kila mtu ana wasiwasi kuhusu mvua ambazo huchukuwa muda mrefu bila ya kunyesha.

Ukosefu wa mvua ambao mwishowe huleta ukame na njaa umechangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za binadamu ambazo zinaongezeka kwa haraka siku hadi siku. Shughuli hizo kwa upande mmoja zimeonekana kama za kimaendeleo, hupelekea kuongezeka kwa matumizi ya maliasili. Mifano mbalimbali ambayo inaonesha matumizi hayo ni pamoja na ujenzi wa nyumba nyingi zaidi, kupata nishati ya kutosha kwa ajili ya kupikia na upatikanaji wa mbao na magogo kwa wingi kwa matumizi ya ndani na hata ya nje ya nchi.

Hata hivyo, ili maendeleo haya yawe na mwelekeo chanya jamii inalazimika kupanda miti kwa wingi ili kukidhi mahitaji hayo. Aidha ni vyema kuzingatia kuwa ukataji wa miti ni chanzo kikubwa cha mito na vijito kuwa na maji haba au kukauka kabisa.

1. Maswali

i. Shughuli za binadamu huleta athari gani kwa jamii?

______________________________________________

______________________________________________

ii. Taja mifano miwili (2) ya shughuli za kibinadamu ambazo hupelekea athari kwa jamii.

______________________________________________

______________________________________________

iii. Bainisha sababu inayopelekea mito na vijito kuwa na maji haba au kukauka.

______________________________________________

______________________________________________

iv. Jamii inashauriwa nini ili kukabiliana na ongezeko la ukataji wa miti?

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

v. Tunga sentensi moja (1) kwa kila neno lililopigiwa mstari.

a) ____________________________________________________________

b) ____________________________________________________________

c) ____________________________________________________________

d) ____________________________________________________________

2. Fupisha aya ya pili ya habari uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi ishirini (20).

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

## SEHEMU B: (Alama 40)

## SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Jibu maswali MANNE (4) katika sehemu hii. Swali la sita (6) ni la lazima.

3. a) Ainisha maneno yanayounda sentensi zifuatazo:

Kwa mfano:

Mvua inanyesha.
N T

i. Wewe umenisaidia sana.

ii. Baskeli yangu imetoboka mpira.

iii. Wageni walikuwa wanataka kukusalimia.

b) Eleza maana ya istilahi zifuatazo:

i. Tungo

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

ii. Kirai

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

4. a) Ainisha kiunganishi kilichopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:

Kwa mfano:

Analia kwa kuwa ana huzuni.

Kiunganishi sababu

i. Sitokula wali wala muhogo.

______________________________________________________________

ii. Nilimtembelea kwao lakini sikumkuta.

______________________________________________________________

iii. Simba na chui ni wanyama hatari.

______________________________________________________________

b) Toa mfano mmoja mmoja (1) kwa kila aina za sentensi zifuatazo:

i. Sentensi shurtia

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

ii. Sentensi changamano

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

5. a) Eleza umuhimu wa ufupisho wa habari.

i. ____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

ii. ____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

iii. ____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

b) Andika nambari zifuatazo kwa maneno.

i. 435,040

____________________________________________

____________________________________________

ii. 3,100,009

____________________________________________

____________________________________________

6. a) Andika sentensi zifuatazo kwa lugha ya Kiswahili.

i. Our government has increased the price of seaweed and cloves.

____________________________________________

____________________________________________

ii. Yesterday I completed my homework at quarter to eleven.

____________________________________________

____________________________________________

iii. Octopuses and crabs are different.

____________________________________________

____________________________________________

b) Andika maneno yafuatayo kwa nambari.

i. Laki nane, elfu tano mia moja na sita.

______________________________________________

ii. Bilioni moja.

______________________________________________

7. a) Eleza kwa ufupi lahaja zifuatazo za Kiswahili:

i. Kihadimu

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

ii. Kimrima

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

iii. Kiunguja

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

b) Andika neno la Kiswahili sanifu kwa lahaja zifuatazo:

| | LAHAJA | KISWAHILI SANIFU |
|---|---|---|
| i. | Chifyu | |
| ii. | Munyu | |

SEHEMU C: (Alama 30)

FASIHI

Jibu maswali MAWILI (2) katika sehemu hii.

8. Tunga beti mbili (2) za shairi la kimapokeo, kisha onesha kina cha kati, kina cha mwisho na idadi ya mizani za shairi hilo.

9. a) Eleza maana ya istilahi zifuatazo:

i. Ushairi

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

ii. Mshororo

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

iii. Urari

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

b) Chagua maana sahihi ya misemo kutoka kwenye mabano.

i. Kushikwa sikio

________________________________________________

(Kuumwa na sikio, kuonywa, kukamatwa sikio)

ii. Kuwa macho

________________________________________________

(kuwa mpole, kuwa hujalala, kuwa makini)

10. Andika tamthiliya fupi uipendayo.

Nambari ya Mtahiniwa ______________________

SEHEMU D: (Alama 15)

UTUNGAJI

Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.

11. Andika Insha ya maneno kati ya 120 – 130 yenye kichwa cha habari, "UGONJWA WA MALARIA".

12. Jaalia wewe ni mfugaji bora wa kuku, tayarisha tangazo la biashara kwa njia ya bango ili kutangaza bidhaa zinazotokana na ufugaji wako.

..............................................